


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO

24 MEI, 2019



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO – TAREHE 24 MEI, 2019

I. DUA:

II. HATI ZA KWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MADINI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

287. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mkoa wa Tanga ndiyo Mkoa wenye Halmashauri nyingi zaidi kwa sasa ukiwa na jumla ya Halmashauri kumi na moja:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuugawa Mkoa huo ili kurahisisha shughuli za utawala na maendeleo.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**288. MHESHIMIWA BUPE NELSON
MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa itaanza kujengwa.

**289. MHESHIMIWA SONIA JUMAA MAGOGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha au kurekebisha Sheria ambazo zinaonekana kuitwa na wakati au kuchocheara ukandamizaji kwa Mama na Mtoto.

WIZARA YA KILIMO:

**290. MHESHIMIWA PAULINE PHILIP GEKUL
(BABATI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Shamba la Singu Estate litarudishwa kwa Wananchi wa Kata ya Sigino kama alivyoahidi Mhe. Waziri Mkuu alipofanya ziara katika Jimbo la Babati Mjini mwaka 2017.

291. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASSIN CHIKAMBO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Serikali iliivunja Bodi ya Korosho na majukumu yake sasa yanatekelezwa na Bodi ya Mazao mchanganyiko:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuunda tena Bodi ya Korosho na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kama ilivyo kwa Mazao mengine.

WIZARA YA MAJI:

292. MHESHIMIWA AUGUSTINE VUMA HOLLE (KASULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Kata ya Buhoro Wilayani Kasulu ina shida kubwa ya maji:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa mradi wa visima vikubwa viwili kwenye Kijiji cha

Shunga ili kuwasaidia akina Mama wanaoteseka.

293. MHESHIMIWA JOYCE BITTA SOKOMBI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Mkoa wa Mara unakabiliwa na changamoto ya maji safi na salama kwa muda mrefu hasa katika Jimbo la Musoma Vijijini, Wilaya ya Bunda, Jimbo la Serengeti, Butiama na Rarya licha ya kwamba Mkoa huo umezungukwa na Ziwa Victoria:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inasambaza mabomba ya maji katika maeneo yenye ukosefu wa maji.

294. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Jimbo la Bunda hususan Kata saba za Mugeta, Mihingo, Kitale, Nyamuswa, Nyamang'uta, Hunyari na Salama zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji ya kunywa; Serikali ilishalionna hilo na kuapeleka Wataalam wake kufanya survey katika Kata hizo:-

Je, baada ya survey hiyo nini kimeamuliwa na Serikali.

WIZARA YA NISHATI:

295. MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (KIBAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Tatizo la kupungua na kukatika kwa umeme bado linaendelea na baadhi ya maeneo hayajafikishiwa umeme mpaka sasa:-

- (a) Je, ni kwanini matatizo ya kukatika au kupungua kwa umeme katika Jimbo la Kibamba halijapatiwa ufumbuzi kinyume na Serikali ilivyoahidi;
- (b) Je, ni maeneo gani katika Jimbo la Kibamba mpaka sasa TANESCO hajafikisha umeme na lini yatafikiwa;
- (c) Je, kuna mkakati gani wa kupunguza gharama kwa Wananchi za kuunganisha umeme au kuwarejeshea wanapovuta wenyewe umbali mrefu.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

296. MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS BUBERWA KAMALA (NKENG):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Kumekuwa na utaratibu

kwa Vyuo Vikuu Tanzania kuajiri Wahadhiri toka nje ya nchi kwa lengo la kukuza tafiti na taaluma katika Vyuo hivyo:-

- (a) Je, katika miaka 10 iliyopita, ni Wahadhiri wangapi wameajiriwa katika Vyuo Vikuu Tanzania;
- (b) Je, ni mafanikio gani kitaaluma na kiutafiti yameletwa na Wahadhiri hao toka nje ya nchi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:-

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
24 MEI, 2019

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE